# ANDIKO LA MRADI

## TAMASHA LA KIMATAIFA LA JULIUS KAMBARAGE NYERERE

### JUKANYE INTERNATIONAL FESTIVAL

JULIUS KAMBARAGE NYERERE
INTERNATIONAL
FESTIVAL

**Waandaaji:**

**JASIRI ARTS & CULTURE INSTITUTION (JACI)**
**Usajili:** Chini ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)

**CATZ COMPANY LIMITED**
**Usajili:** BRELA - **173701225**

**MAKUMBUSHO YA TAIFA LA TANZANIA**
Chini ya:WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

**Mlezi wa Tamasha:** Bi. Anna Julius Nyerere

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM

JASIRI ARTS & CULTURE INSTITUTION (JACI)
**S.L.P 38012, Dar es Salaam, Tanzania**
**Simu: 0789 388232 / 0673 023547**
**Email: jukanyefestival@gmail.com**

MAKUMBUSHO YA TAIFA LA TANZANIA (NMT)
**S.L.P S.L.P 511 Mtaa wa Shaaban Robert**
**Posta - Dar es salaam**
**Barua pepe: dg@nmt.go.tz**
**Simu: +255 715 865662**

CATZ COMPANY LIMITED
**S.L.P 19601, Dar Es Salaam Tanzania,**
**Simu: +255 746 174403 / +255 673196681**
**Email: catzcom2024@gmail.com**

**WASHIRIKA:**

| | | |
|---|---|---|
| **Wizara ya Maliasili na Utalii** | Makumbusho ya Taifa (NMT) | Ushirikishwaji wadau wa utalii |
| **Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo** | Kituo Cha Urithi Wa Ukombozi Wa Bara La Afrika, BASATA | Maonesho ya urith wa ukombozi, Sanaa na utamaduni |
| **Wizara Ya Nishati** | | Maonesho ya nishati salama ya kupikia |
| **Wizara ya Viwanda na Biashara** | SIDO | Monesho ya maendeleo ya viwanda |
| **Wizara ya Ulinzi** | JWTZ (Sanaa) | Maonesho, ukombozi, Vita vya Kagera |
| **Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari** | | Uwezeshaji miundo mbinu |
| **Wizara ya utalii na Mambo ya Kale - Zanzibar** | Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale. | Maonesho ya makumbusho ya Zanzibar |
| **Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki** | | Ushirikiano wa Kimataifa |
| **TAMISEMI** | | Ushirikiano na uhamasishaji Kitaifa |
| **WADHAMINI, WAFADHILI, JAMII YA NDANI YA NCHI NA JAMII YA KIMATAIFA** | | Uwezeshaji, uhamasishaji na ushiriki |

## YALIYOMO


### A. KUHUSU JUKANYE

**(I) UTANGULIZI:**

- Jukanye
- Tarehe
- Kauli Mbiu
- Lengo Kuu
- Dhima
- Urithi Wa Mwalimu Nyerere
- Viongozi waalikwa
- Washiriki wengine

**(II) MALENGO MAHSUSI:**
**(III) VIPENGELE VYA TAMASHA**

### B. TUZO

- Madhumuni na Falsafa ya Tuzo
- Usimamizi wa tuzo
- Makundi ya Tuzo
- Utoaji wa Tuzo

### C. BAJETI

I. BAJETI NA VYANZO VYA MAPATO
II. FURSA NYINGINE ZA TAMASHA
III. FAIDA ZITAKAZO TOKANA NA TAMASHA
IV. UONGOZI NA UTEKELEZAJI
V. USIMAMIZI WA HATARI ENDELEVU
VI. HITIMISHO

# A. KUHUSU JUKANYE

## UTANGULIZI

**TAMASHA LA KIMATAIFA LA JULIUS KAMBARAGE NYERERE ( JULIUS KAMBARAGE NYERERE INTERNATIONAL FESTIVAL ) JUKANYE:**

**Taasisi ya JASIRI ARTS & CULTURE (JACI)** ya jijini Dar es Salaam, iliyosajiliwa chini ya BASATA, ikijishughulisha na sanaa, utamaduni na uratibu wa matukio ya kijamii na kihistoria, na **CATZ Company Limited** – ya jijini Dar es Salaam, iliyosajiliwa BRELA (173701225), inayojishughulisha na ubunifu, uandishi na uzalishaji wa maudhui ya kijamii na kiutamaduni, kwa Kushirikiana na **Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania (NMT)** – chombo cha umma kilicho chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kinachohusika na kuhifadhi na kuendeleza urithi wa kihistoria wa taifa, kwa pamoja wanatangaza maandalizi ya Tamasha la Kimataifa la JUKANYE 2027, tukio la kila baada ya miaka miwili linaloenzi urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Tamasha hili linaandaliwa kwa ushirikiano wa Karibu na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), KITUO cha Urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika (ALH) pamoja na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO). Tamasha hili litafanyika Jijini Arusha katika viwanja vya Kisongo kuanzia tarehe 17, Julai 2027 – 01 August 2027. likihusisha Utalii – Maonyesho mbalimbali, Warsha, Michezo, Utamaduni, Huduma za Kijamii, Burudani, na utoaji wa Tuzo).

**Kaulimbiu:** "Uchumi wa Afrika Utaimarishwa na Waafrika Kupitia Umoja"

**Lengo Kuu:** Kuenzi viongozi wa Afrika waliopigania uhuru na kuhamasisha uzalendo kwa kizazi cha sasa.
**Dhima na Maono:** Kuwa jukwaa la kuenzi historia ya ukombozi wa Afrika kupitia mchango wa viongozi wake, wakiongozwa na Mwalimu Nyerere, kupitia utalii, sanaa, makongamano, maonesho, na burudani za kitamaduni na utoaji wa tuzo.
**Urithi wa Mwalimu Nyerere:** Kuendeleza maono na misingi ya mshikamano, utu, amani, ukweli, unyenyekevu, na upendo kwa watu wote; kuhakikisha fikra na maadili haya yanatunzwa kwa vizazi vijavyo.

**Viongozi Wakuu Wanaotarajiwa Kualikwa**

- **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mgeni Rasmi wa Ufunguzi)
- **Mhe.** haled El-Enany **Mkurugenzi Mkuu (Director-General) wa UNESCO**.(Mgeni Rasmi wa Utoaji wa Tuzo za Heshima)
- **Kapteni Ibrahim Traoré** – Rais wa Mpito wa Burkina Faso (Mgeni wa Kufunga Tamasha)

**Washiriki:** Viongozi / wawakilishi wa nchi zote za Afrika, mataifa rafiki, wadau wa kimataifa, mashirika ya elimu, maendeleo, utamaduni, taasisi za urithi wa ukombozi wa Afrika na wananchi wote wa ndani na nje ya Tanzania.

## (II) MALENGO MAHSUSI

1. Kuendeleza maono ya Mwalimu Nyerere juu ya umoja na maendeleo, na Kulinda mazingira.
2. Kuimarisha uzalendo, amani, mshikamano, na haki za kijamii.
3. Kuhifadhi historia ya ukombozi na kuelimisha vizazi.
4. Kukuza uchumi, ubunifu, ajira, na ushiriki wa vijana.
5. Kutangaza Kiswahili, utamaduni, na urithi wa Afrika.

## (III) VIPENGELE VYA TAMASHA

1. Onesho la mchango wa Mwalimu Nyerere katika Uhuru, utamaduni na maendeleo
2. Maonyesho ya makumbusho ya viongozi wa Afrika na mchango wao.
3. Burudani za muziki wa asili na kisasa kutoka mataifa mbalimbali.
4. Michezo ya kuigiza historia ya ukombozi.
5. Maonyesho ya mavazi na utamaduni wa nchi washiriki.
6. Makongamano mbalimbali kujadili maendeleo ya Afrika na utatuzi wa chnagamoto za vijana.
7. Kliniki za afya kwa jamii.
8. Ziara za kihistoria na kitalii (Butiama, Tabora, Dar es Salaam, Zanzibar, na mikoa ya Kusini).
9. Kuhamasisha matumizi ya nishati salama za kupikia.
10. Uzinduzi wa makala maalum kuhusu Mwalimu Nyerere.
11. Madarasa ya Kiswahili kwa wageni.
12. Maonesho ya Biashara, Technolojia na Viwanda
13. **Utoaji wa tuzo mbalimbali kama ifuatavyo:**

# B. Tuzo

## 1. Madhumuni na Falsafa ya Tuzo

Tuzo na Heshima za Tamasha la Kimataifa la Julius Kambarage Nyerere (JUKANYE) zimeanzishwa kwa lengo la **kuheshimu urithi wa harakati za ukombozi wa Afrika, ubora wa kitamaduni, uongozi wa kimaadili, na mshikamano wa kimataifa**, kwa kuzingatia misingi na maadili ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Tuzo hizi zinatumika kama **jukwaa lisilo la kisiasa, linaloongozwa na maadili**, kwa madhumuni ya kulinda kumbukumbu ya kihistoria, kuhamasisha kizazi cha sasa na kijacho, na kuimarisha umoja wa Kipaanafrika kupitia utambuzi wa watu binafsi, harakati, tamaduni, na mataifa yaliyotoa mchango muhimu katika uhuru, utu, na maendeleo ya Afrika.

Tuzo na heshima zote chini ya JUKANYE ni **za heshima na ishara tu kwa asili yake**. Hazimaanishi kuunga mkono kisiasa, kutathmini serikali zilizopo madarakani, wala kuhusishwa na misimamo ya kisiasa.

## Tamko la Kutoegemea Upande wa Kisiasa na Maadili

*"Tuzo na Heshima za Tamasha la Kimataifa la Julius Kambarage Nyerere sio za kisiasa, zinazoongozwa na maadili, na zinajikita katika urithi wa kihistoria, mchango wa kitamaduni, na mshikamano wa Kipaanafrika. Hazimaanishi kuunga mkono kisiasa wala kutathmini uongozi wa kisiasa wa sasa."*

## 2. Usimamizi wa Tuzo

Ili kuhakikisha **uaminifu, heshima, na uadilifu wa kihistoria**, Tuzo za JUKANYE zitasimamiwa chini ya uangalizi wa **Baraza Huru la Tuzo la JUKANYE**.

**Baraza la Tuzo litakuwa na majukumu ya:**

- Kuthibitisha makundi ya tuzo na maelezo ya heshima (citations)
- Kuhakikisha usahihi wa kihistoria na uwiano
- Kulinda na kuendeleza maadili ya Uafrika, umoja, na uadilifu wa kitamaduni
- Kulinda tabia isiyo ya kisiasa ya Tamasha

Baraza litaundwa na wawakilishi wanaoheshimika kutoka:

- Taasisi za utamaduni na urithi wa kihistoria
- Wasomi na wataalamu wa masomo ya Kipaanafrika
- Makumbusho ya Taifa ya Tanzania
- Kamati kuu / Sekretarieti ya JUKANYE

## 3. Makundi ya Tuzo na Heshima

Tuzo za JUKANYE zimegawanywa katika **makundi mawili makuu**:

1. **Tuzo za Kihistoria na Urithi** (kwa waliotangulia mbele ya haki, zisizo na utata)
2. **Heshima za Uongozi na Utamaduni wa Kisasa** (za heshima ya kifasihi na kimaadili)

## KUNDI LA KWANZA: TUZO ZA KIHISTORIA NA URITHI

*(Kwa waliotangulia mbele ya haki, na walio hai)*

### 3.1 Tuzo ya Heshima ya Ukombozi wa Afrika

Tuzo hii inawatambua **viongozi wa harakati za ukombozi wa Afrika waliotangulia mbele ya haki na walio hai**, ambao kwa uongozi wao, kujitolea, na maono yao yalichangia kwa kiasi kikubwa mapambano dhidi ya ukoloni, ubaguzi wa rangi (apartheid), na mifumo ya dhuluma, na hivyo kuchangia uhuru wa kisiasa na heshima ya Afrika.
Tuzo hii inalenga **kuhifadhi urithi wa kihistoria** wa viongozi hao kama sehemu ya kumbukumbu ya pamoja ya bara la Afrika.

Watakaopata tuzo ya **African Libertion Award of honor ya** JUKANYE INTERNATIONAL FESTIVAL – 2027; ni viongozi kumi (10) kutoka katika kundi hili:

| | NCHI | KIONGOZI | HALI |
|---|---|---|---|
| 1 | Tanzania | Mwalimu Julius Kambarage Nyerere | Marehemu |
| 2 | Zanzibar | Abeid Amani Karume | Marehemu |
| 3 | Msumbiji | Samora Machel | Marehemu |
| 4 | Zambia | Kenneth Kaunda | Marehemu |
| 5 | Angola | Agostinho Neto | Marehemu |
| 6 | Botswana | Seretse Khama | Marehemu |
| 7 | Kenya | Jomo Kenyatta | Marehemu |
| 8 | Uganda | Milton Obote | Marehemu |
| 9 | Ghana | Kwame Nkrumah | Marehemu |
| 10 | Afrika Kusini | Nelson Mandela | Marehemu |
| 11 | Zimbabwe | Robert Mugabe | Marehemu |
| 12 | Algeria | Ahmed Ben Bella | Marehemu |
| 13 | Guinea | Ahmed Sékou Touré | Marehemu |
| 14 | Namibia | Sam Nujoma | Marehemu |
| 15 | Malawi | Hastings Kamuzu Banda | Marehemu |
| 16 | Ethiopia | Haile Selassie | Marehemu |
| 17 | Burkina Faso | Thomas Sankara | Marehemu |
| 18 | Nigeria | Nnamdi Azikiwe | Marehemu |
| 19 | Senegal | Léopold Sédar Senghor | Marehemu |
| 20 | Cameroon | Ahmadou Ahidjo | Marehemu |
| 21 | Congo (DRC) | Patrice Lumumba | Marehemu |

### 3.2 Tuzo ya Mama Afrika ya Ukombozi na Urithi

Tuzo hii inawaheshimu **wanawake wa historia ya ukombozi wa Afrika**, wakiwemo wake wa viongozi wa ukombozi na wanaharakati wa kike, waliotoa mchango mkubwa katika harakati za ukombozi, uhamasishaji wa jamii, na kulinda maadili na utambulisho wa Kiafrika.

Tuzo hii inatambua uongozi wa wanawake, ustahimilivu wao, na mchango wao ambao mara nyingi haukutambuliwa vya kutosha katika harakati za ukombozi na ujenzi wa mataifa ya Afrika.

Watakao pata tuzo ya **mama afrika for liberation and legacy ya** JUKANYE INTERNATIONAL FESTIVAL – 2027; ni

| | NCHI | KIONGOZI | HALI |
|---|---|---|---|
| 1 | Afrika Kusini | Winnie Madikizela-Mandela | Marehemu |
| 2 | Nigeria | Funmilayo Ransome-Kuti | Marehemu |
| 3 | Tanzania | Maria Nyerere | Hai |
| 4 | Msumbiji | Josina Machel | Marehemu |
| 5 | Msumbiji | Graça Machel | Hai |
| 6 | Angola | Queen Nzinga – (Karne ya 17) | Marehemu |
| 7 | Kenya | Mama Ngina Kenyatta | |
| 8 | Tanzania | Bibi Titi Mohamed | Marehemu |

### 3.3 Tuzo ya Hekima ya Ukombozi

Tuzo hii hutolewa kwa **viongozi wa kidini na kimaadili waliotangulia mbele ya haki**, waliotoa uongozi wa kimaadili, mwongozo wa kiroho, na ujasiri wa dhamira wakati wa harakati za ukombozi wa Afrika.

Inawaheshimu viongozi waliotumia imani, dhamira, na mamlaka ya maadili kuhamasisha mapambano dhidi ya dhuluma na kukuza amani, utu wa binadamu, na umoja.

Watakaopata Tuzo hii ya **WISDOM OF LIBERATION ya** JUKANYE INTERNATIONAL FESTIVAL – 2027; ni

| | NCHI | KIONGOZI | HALI |
|---|---|---|---|
| 1 | Afrika Kusini | Archbishop Desmond Tutu | Marehemu |
| 2 | Ethiopia | Abuna Theophilos | Marehemu |
| 3 | Zimbabwe | Bishop Abel Muzorewa | Marehemu |

## 3.4 Heshima ya Mshikamano wa Kimataifa

Heshima hii ni kwa **mataifa yaliyo nje ya bara la Afrika** ambayo kihistoria yalitoa msaada wa kisiasa, mali, au kimaadili kwa harakati za ukombozi wa Afrika wakati wa mapambano dhidi ya ukoloni na ubaguzi wa rangi.
Heshima hii inajikita kikamilifu katika **mshikamano wa kihistoria**, kwa kutambua mchango uliotolewa katika enzi ya ukombozi wa Afrika.

Watakaopata Tuzo hii ya **GLOBAL SOLIDARITY AWARD** ya JUKANYE INTERNATIONAL FESTIVAL – 2027; ni

- **China**
- **Urusi**
- **Cuba**
- **Sweden**



## KUNDI LA PILI: HESHIMA ZA UONGOZI NA UTAMADUNI ZA KISASA

*(Za heshima, zinazoongozwa na maadili)*

### 3.5 Heshima ya Uongozi na uzalendo kwa Bara la Afrika

Hii ni **heshima ya kifasihi na kiishara**, si tuzo ya kisiasa.
Inawatambua **baadhi ya Wakuu wa Nchi wa Afrika waliopo madarakani**, kwa kuzingatia mchango wao katika:

- Kukuza uzalendo na kuchochea maendeleo ya Bara la Afrika
- Kuimarisha utulivu wa kikanda na umoja
- Kukuza mazungumzo, ujenzi wa amani, na mshikamano wa Afrika

Heshima hii ni ya kiishara, inaonyesha heshima kwa nafasi ya uongozi na mchango katika ushirikiano wa bara, bila kuashiria kuunga mkono kisiasa.

Watakaopata Tuzo hii ya **CONTEMPORARY PRESIDENTS AWARD ya** JUKANYE INTERNATIONAL FESTIVAL – 2027 ni;

| | NCHI | KIONGOZI | HALI |
|---|---|---|---|
| 1 | Tanzania | Dr. Samia Suluhu Hassan | Rais |
| 2 | Uganda | Yoweri Kaguta Museven | Rais |
| 3 | Rwanda | Paul Kagame | Rais |
| 4 | Burkina Faso | Ibrahim Traoré | Rais |
| 5 | Benin | Patrice Talon | Rais |
| 5 | Namibia | Netumbo Nandi-Ndaitwah | Rais |
| 5 | Botswana | Duma Gideon Boko | Rais |
| 5 | Ghana | John Dramani Mahama | Rais |

## 3.6 Sauti ya Ukombozi – Heshima ya Muziki na Utamaduni

Heshima hii inawatambua **wasanii wa muziki na wana-utamaduni kutoka Afrika na dunia kwa ujumla**, ambao kazi zao za kisanii zimehamasisha fikra za ukombozi, utambulisho wa Kipaanafrika, haki ya kijamii, na umoja katika vizazi mbalimbali.
Heshima hii inaadhimisha utamaduni kama **nyenzo ya uhamasishaji, mapambano, uponyaji, na muunganiko wa bara la Afrika**.
Uteuzi unazingatia mchanganyiko wa:

- Ushiriki wa umma
- Uthibitisho wa jopo la wataalamu wa maswala ya muziki na utamaduni

ili kuhakikisha **uadilifu wa kisanii na thamani ya kitamaduni**.

**(THE VOICE OF LIBERATION):**

Tuzo hizi zimegawanywa katika makundi, na mshindi mmoja atachaguliwa kutoka kila kundi kupitia kura za mtandaoni kwenye Tovuti na App ya JUKANYE. Kila mshindi atapokea tuzo pamoja na fedha taslimu kulingana na kundi lake.

| | | | |
|---|---|---|---|
| A. | KUNDI LA WANAMUZIKI WA NJE YA AFRIKA - ZAMANI | | |
| B. | KUNDI LA WANAMUZIKI WA NJE YA AFRIKA - SASA | | |
| C | KUNDI LA WANAMUZIKI WA AFRIKA - ZAMANI | | |
| D. | KUNDI LA WANAMUZIKI WA AFRIKA - SASA | | |
| E | KUNDI LA WANAMUZIKI WA TANZANIA - ZAMANI | | |
| F | KUNDI LA WANAMUZIKI WA TANZANIA - SASA | | |

15

## 4. Utoaji wa Tuzo na Itifaki

- **Tuzo za Kihistoria na Urithi** zitatolewa wakati wa vipindi maalum vya kitamaduni na urithi wa kihistoria ndani ya Tamasha.
- **Heshima za Uongozi na Utamaduni wa Kisasa** zitatolewa wakati wa hafla za ngazi ya juu za heshima, kwa kuzingatia itifaki za kidiplomasia na za kiserikali.

Hafla zote zitazingatia:

- Heshima na hadhi
- Alama na ishara za kitamaduni
- Viwango vya itifaki za kimataifa

## 5. Urithi wa Tuzo

Kupitia Tuzo hizi, JUKANYE inalenga:

- Kulinda na kurithisha historia ya ukombozi wa Afrika
- Kuheshimu ujasiri wa kimaadili na ubora wa kitamaduni
- Kuhamasisha vijana na vizazi vijavyo
- Kuimarisha utambulisho wa pamoja na umoja wa Afrika

*Tuzo hizi zinasimama kama* ***heshima hai kwa misingi na maadili ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere****, na safari ya pamoja ya Afrika kuelekea utu, umoja, na maendeleo endelevu.*

# C. BAJETI

## (I) BAJETI NA VYANZO VYA MAPATO:

- Bajeti ya tamasha: takriban **Shilingi Bilioni 3.35** ambazo zitatumika kughramia tamasha lote kuanzia; maandalizi ya awali, utambulisho wa Tamasha kupitia vyombo vya habari na uzinduzi wa tamasha (August - Octoba 2026 na tamasha kuu Julai / August 2027. Gharama zitahusisha viwanja vya maonesho, mahema na majukwaa, vyombo vya muziki, gharama za wasanii, usafiri, teknolojia, usalama,Protocol facilitations, tuzo na matangazo, Uzalishaji wa Makala rasmi ya Mwalimu Nyerere na malipo ya watendaji.
- Mapato yatatumika kuendeleza tamasha lijalo, kusaidia vijana, na kuimarisha Makumbusho ya taifa kwa kuiweka katika mfumo wa kigitali (Digitization of the National Museum sites and monuments).

**Vyanzo vya Mapato:**

1. Wadhamini na wafadhili (Platinum, Gold, Silver, Bronze)
2. Michango ya nchi zinazonufaika
3. Michango ya wadau binafsi na taasisi
4. Uuzaji wa mahema ya maonyesho
5. Bidhaa rasmi za tamasha (Vitabu, Vitenge, Mashati, kofia, Fulana (T-shirts) nk.)

**Muhtasari wa Gharama**

• **Jumla:** TZS 3,350,000,000 (Wadhamini wakuu, Nchi shiriki, Mashirika ya mbalimbali ya ndani na nje ya Tanzania na Michango ya Marafiki wa Jukakanye

• Wadhamini wakubwa watapata Mabanda ya maonyesho, fursa za kipekee za kushiriki na kutangaza bidhaa ama huduma zao katika tamasha na kupitia vyombo vya habari vitakavyo kuwa vinatangaza tukio hili kabla na wakati wa tukio.

• Nchi Shiriki zitapata Mabanda ya maonyesho, fursa za kipekee za kushiriki na kutangaza nchi zao, bidhaa ama tamaduni zao zao katika tamasha na kupitia vyombo vya habari vitakavyo kuwa vinatangaza tukio hili kabla na wakati wa tukio.

• Taasisi mbalimbali zitapata nafasi za kujitangaza lakini pia kutambulika kuwa wawezeshaji wa tukio hili kubwa na la kihistoria

**Wachangiaji Marafiki wa Jukanye**

Tunawakaribisha watu binafsi, makundi, na taasisi kuchangia kwa moyo wote katika Tamasha la JUKANYE INTERNATIONAL FESTIVAL kama **Wachangiaji Marafiki wa Jukanye**. Michango ya Wachangiaji Marafiki inaanzia **shilingi za Kitanzania 500,000 (LAKI TANO)** na kuendelea, bila kikomo cha juu, na kila mchango utasaidia moja kwa moja kufanikisha maandalizi na utekelezaji wa tamasha hili muhimu.

Tamasha hili linatarajiwa kukusanya watu zaidi ya 200,000 katika siku zote za tamasha, na kufuatiliwa na mamilioni ya watu kupitia vyombo vya habari, kutakuwa na vipindi maalumu katika luninga vitakavyokuwa vinatangaza maudhui ya tamasha, na siku ya ufunguzi, na siku ya kufunga matukio yataonyeshwa Mubashara(Live) kupitia Luninga na Radio.

- **Kwa Nini Kushirikiana na JUKANYE?**
- • Tamasha la kimataifa lenye hadhira kubwa ya vijana, familia na wadau wa maendeleo.
- • Kupata 'Brand Visibility' katika nyanja za kitaifa na kimataifa kwa kuunganishwa na viongozi, wadau wakubwa, wawekezaji na balozi.
- • Nafasi ya kuonyesha na kuuza bidhaa au huduma kwa maelfu ya washiriki na hivyo kuongeza mauzo, hadhi ya chapa (brand) katika soko la Afrika Mashariki na duniani kote.

**3. Thamani kwa Mdau**

Kwa kushiriki katika JUKANYE Festival 2026 / 2027, mdau atanufaika kwa:

- Ufikiaji wa maelfu ya washiriki wa ndani na wa kimataifa, Kuongeza mauzo na utambulisho wa bidhaa/huduma
- Ushiriki katika tukio lenye hadhi ya kitaifa na kimataifa
- Mtandao mpya wa kibiashara na kijamii

**4. Wito Kwa Ushiriki**

Fursa hizi zimeandaliwa kwa uwazi, mpangilio na usawa ili kuhakikisha kila mdau, mkubwa au mdogo, anapata nafasi ya kushiriki na kunufaika.

Tunawaalika wadau wote kuchangamkia fursa hizi kwa kuwasiliana na Kamati ya Maandalizi ya JUKANYE Festival 2026 kwa ajili ya:

- Kuchagua eneo au fursa husika, Kujadiliana masharti na Kukamilisha usajili

## (IV) FAIDA ZITAKAZO TOKANA NA TAMASHA

**Faida za Kiuchumi kwa Tanzania:**

- **Muda Mfupi:** Kuongezeka kwa mapato sekta za malazi, usafiri, chakula; ajira za muda mfupi; uuzaji wa bidhaa za mikono; kodi na tozo zaidi kwa serikali.
- **Muda Mrefu:** Kukuza utalii wa kihistoria na kiutamaduni; kuvutia uwekezaji; kuimarisha utambulisho wa Tanzania kimataifa; kuendeleza vipaji vya vijana na uchumi wa ubunifu.

**Maeneo Yanayotarajiwa Kunufaika zaidi:** Butiama, Dar es Salaam, Zanzibar, Tabora, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, mikoa ya Kusini, na mikoa mingine itakayoshiriki.

**Faida kwa Wadhamini:** Utambulisho wa kitaifa na kimataifa, nembo kwenye jukwaa, fulana, mabango, mitandao ya kijamii, nafasi za biashara, mialiko maalum.

**Faida za kuwa Mchangiaji Marafiki:**

- Kutajwa rasmi katika kumbukumbu za tamasha kama marafiki wa tukio
- Kupokea taarifa maalumu za maendeleo ya tamasha
- Kushiriki katika mshikamano wa kijamii unaoleta maendeleo ya Afrika kupitia urithi wa Mwalimu Nyerere.
- Fursa ya kushiriki katika hafla za tamasha kama washirika wa heshima.(Vigezo na maharti kuzingatiwa)

## (V) UONGOZI NA UTEKELEZAJI

Tamasha la JUKANYE litaandaliwa na Jasiri Arts & Culture Institution (JACI) na CATZ Company Limited, kwa ushirikiano na Makumbusho ya Taifa ya Tanzania (NMT) chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii.
Utekelezaji utaongozwa na muundo wa uongozi wa wadau mbalimbali unaojumuisha:

**Kamati ya Uongozi wa Tamasha (Kamati Kuu)**

**Sekretarieti ya Tamasha**

- Kamati ya Fedha
- Kamati ya ufundi program, na ushirikiano
- Kamati ya ulinzi, Itifaki na Usalama
- Kamati ya Masoko
- Kamati ya Habari na Matangazo
- Kamati ya ufuatiliaji,tathmin na kujifunza (MEL)

**Kamati Ndogo**

- Kamati ya Muziki na burudani
- Kamati ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika
- Kamati ya Urithi wa Mwalimu Nyerere
- Kamati ya Utalii
- Kamati ya Usafiri
- Kamati ya Maonyesho Mitindo, Mavazi na Utamaduni
- Kamati ya Makongamano na Majadiliano ya Kimkakati
- Kamati ya Afya na Ustawi wa Jamii
- Kamati ya Nishati Safi na Mazingira
- Kamati ya Tuzo na Utambuzi
- Kamati ya Kiswahili na Diplomasia ya Lugha
- Kamati ya Filamu, Hifadhi ya Kumbukumbu na Uzalishaji wa Maudhui

Kamati zinaweza kupungua ama kuongezeka kwa kuundwa ama kufutwa na kamati kuu.

## (VI) USIMAMIZI WA HATARI ENDELEVU

Hatari zinazoweza kujitokeza ni pamoja na changamoto za kiutendaji, upungufu wa rasilimali, na mabadiliko ya mazingira ya nje. Hatua za kukabiliana nazo zitahusisha mipango ya mapema, ushirikiano mpana na wadau mbalimbali, uhamasishaji wa rasilimali kwa awamu, na uratibu madhubuti.

Uendelevu wa Tamasha utahakikishwa kwa kuimarisha ushirikiano wa kitaasisi, kuandaa na kuhifadhi bidhaa za maarifa na nyaraka, kuoanisha utekelezaji wa Tamasha na mikakati ya kitaifa ya maendeleo ya utamaduni na utalii, pamoja na kuliimarisha JUKANYE kama jukwaa la kudumu la Kiafrika linalofanyika kila baada ya miaka miwili.

## (VII) HITIMISHO - MWALIKO RASMI WA USHIRIKIANO:

• **HITIMISHO:**

JUKANYE INTERNATIONAL FESTIVAL ni dira ya kurithisha historia, kulinda utambulisho wa Mwafrika, kukuza ushirikiano wa bara letu, na kuitangaza Tanzania kama nguzo ya maendeleo ya ki-Afrika. Tunakaribisha ushirikiano wa dhati kutoka
kwa Serikali na taasisi zake, nchi mbalimbali hasa wanufaika wa Tamasha hili, mashirika ya ndani na nje, wadau mbalimbali wa ndani na wa Kimataifa, vyuo vikuu, taasisi za kifedha na watu binafsi katika kufanikisha tukio hili la kihistoria.

***Tunathamini kila mchango (mali na ushauri), Jiunge nasi, tuendeleze urithi wa ukombozi wa Afrika pamoja!***

WASILIANA NASI KWA:

- Kudhamini, Kufadhiri, kusaidia kwa hari, mali na ushauri
- Kushiriki , kukodi Vizimba vya maonyesho ama kutoa huduma nyingine katika maonesho
- Kununua Bidhaa za Tamasha

**Kwa Taarifa Zaidi Tembelea** https://www.jukanye.com **Ama Tuandikie** jukanyefestival@gmail.com

Karibu JUKANYE International Festival

JuKaNye

JULIUS KAMBARAGE NYERERE INTERNATIONAL FESTIVAL

BANGO




JuKaNye
JULIUS KAMBARAGE NYERERE
INTERNATIONAL
FESTIVAL
JuKaNye
ARUSHA
TANZANIA
www.jukanye.com

JASIRI ARTS & CULTURE INSTITUTION (JACI)
**S.L.P 38012, Dar es Salaam, Tanzania**
**Simu:+255 673196681**
**+255 789 388232 / 673 023547**
**Email: jukanyefestival@gmail.com**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM

MAKUMBUSHO YA TAIFA LA TANZANIA (NMT)
**S.L.P S.L.P 511 Mtaa wa Shaaban Robert**
**Posta - Dar es salaam**
**Barua pepe: dg@nmt.go.tz**
**Simu: +255 715 865662**

CATZ COMPANY LIMITED
**S.L.P 19601, Dar Es Salaam Tanzania,**
**Simu: +255 746 174403 / +255 795304403**
**Email: catzcom2024@gmail.com**

**Imeandaliwa na: CATZ COMPANY LIMITED**

**MWISHO**